






Siku moja Akadeli, Lucia,  
Acharait na Maria walienda  
msituni kutafuta matunda.  
Walishikana mikono  
wakavuka mto mkubwa.



Waliufikia mti uliojaa  
matunda mabivu.  
Walikubaliana kuukwea mti  
ule na kuyachuma matunda  
wakiwa wameyafumba  
macho yao.



Hata hivyo, Lucia, Acharait na Maria hawakuyafumba macho yao. Akadeli pekee alifanya hivyo alipokuwa akichuma matunda.




Ilipofika wakati wa  
kuyafumbua macho, Akadeli  
alikuta kwamba alikuwa  
ameyachuma matunda  
mabichi pekee.



Lucia, Acharait na Maria  
walimcheka Akadeli kisha  
wakaondoka kwenda zao  
nyumbani. Akadeli aliyatupa  
matunda yale mabichi  
akaanza kuchuma mabivu.



Muda mfupi baadaye,  
Akadeli alikijaza kikapu  
chake kwa matudna  
mabivu. Alianza kuuvuka  
mto ule mkubwa peke yake.




Akadeli alipokuwa katikati,  
kikapu chake kilimponyoka  
na kuanguka majini.  
Alikasirika sana akaanza  
kulia.




Kabla hajavuka ng'ambo,  
Akadeli alimwona samaki  
ukingoni mwa mto.  
Alimchukua.




Alipokuwa amembeba  
samaki yule, mwewe  
alimnyang'anya na kuruka  
naye.



Akadeli aliona unyoya  
mmoja mrefu uliokuwa  
umeachwa na mwewe.  
Ingawa alikasirika,  
aliuchukua ule unyoya na  
kuendelea na safari yake.



Akadeli aliwapita watu wakisherehekea harusi ya kitamaduni. Wachezaji walivalia nyasi vichwani badala ya manyoya kama ilivyokuwa desturi. Waliuchukua ule unyoya wakampatia fahali mkubwa!



Akadeli alifika nyumbani na fahali wake. Wazazi na jamaa zake walifurahi sana. Lucia, Acharait na Maria walisikitaka kumdanganya Akadeli. Ilikuwa siku ya bahati kwa Akadeli!